# GAFCON IV – TAMKO LA KIGALI

[Kristo] ndiye kichwa cha mwili, yaani cha Kanisa; naye ni mwanzo,
ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote (Wakolosai 1:18).

Salaam kutoka Kigali, Rwanda, ambako Kongamano la Nne la GAFCON limefanyika kuanzia tarehe 17-21 Aprili, 2023, likileta pamoja wawakilishi 1,301 kutoka nchi 52, wakiwemo Maaskofu 315, Wachungaji 456 na walei 531.

Tulishukuru kwa ukarimu wa pekee wa Askofu Mkuu Laurent Mbanda na Kanisa Anglikana Rwanda. Tulisikitishwa sana kusikia juu ya kifo cha Edwin, kijana wa Laurent na mkewe Chantal, na tunaendelea kutoa sala zetu za faraja kwa familia ya Mbanda.

Pia tulipata heshima ya kukaribishwa na kuhutubiwa na Waziri Mkuu wa Rwanda, Mheshimiwa Edouard Ngirente ambaye alizungumza kuhusu kusanyiko letu.

Neno Kuu la Kongamano la 2023 "Twende Kwa Nani" (Yohana 6:68) pamoja na mitaala ya Biblia katika Waraka kwa Wakolosai kwa pamoja vimetuwezesha kulenga kumtazama Yesu, ambaye utimilifu wa Mungu unakaa juu yake katika mwili, Bwana wa uumbaji na kichwa cha mwili wake, 'yaani Kanisa' (Wakolosai 1:15-19; 2:9).

Katika hotuba yake ya ufunguzi, Mwenyekiti wetu alituhimiza tuwe Kanisa lenye toba, Kanisa la upatanisho, Kanisa linalozaa, na lenye bidii katika kuleta faraja. Tunataka kuwa Kanisa la aina hii.

Tulikumbushwa kwamba lengo na Utume wa Kanisa ni kujulisha ulimwengu uliopotea kuhusu utajiri wenye utukufu wa Injili kwa kumtangaza Kristo aliyesulubiwa na kufufuka, na kuishi pamoja kwa uaminifu kama wanafunzi wake.

**Ushirika Wetu Pamoja**

Tulishukuru kwa wema na uaminifu wa Mungu juu ya ushirika wa Gafcon tangu kuanzishwa kwake mwaka 2008, kama ambavyo pia tumefurahia kizazi kipya cha viongozi wanaojitokeza. Ni Mungu anayetuunganisha na yeye mwenyewe na pia anatuunganisha sisi kwa sisi katika nguvu ya Roho Mtakatifu (1 Wakorintho 12:13). Pamoja na kwamba tumetoka katika mazingira na mila tofauti tofauti, tunafurahia umoja wetu ndani ya Kristo pamoja na upendo tunaoshiriki pamoja.

Wengi wetu tunatoka katika mazingira ya mateso au migogoro, tunafahamu kwamba sehemu moja ya mwili ikiumia, wote tunaumia. Baadhi walishindwa kuhudhuria kongamano kwa sababu hiyo. Tuliomba kwa ajili ya ndugu na dada zetu walioko Sudan, na kwa ajili ya Kanisa lililo katika mateso. Vile vile tulisikia shuhuda mbalimbali juu ya nguvu ya Injili katika kubadilisha maisha kupitia katika maombi, ukarimu na huruma ya Wakristo hata katika mazingira hayo ya mateso.

**Mamlaka ya Neno la Mungu**

Mgawanyiko uliopo sasa hivi katika Ushirika wa Waanglikana Ulimwenguni (Anglican Communion) umesababishwa na baadhi kuachana kabisa na Injili ya Bwana wetu Yesu Kristo. Baadhi ya watu katika Ushirika wa Waanglikana Ulimwenguni wamechukuliwa mateka wa falsafa zilizo tupu na za udanganyifu za ulimwengu huu (Wakolosai 2:8). Hali hii ya kushindwa kusikia neno la Mungu ina inahujumu Utume wa Kanisa kwa jumla.

Biblia ni Neno la Mungu lililovuviwa na Mungu na kuandikwa na watu wake waaminifu (2 Tim 3:16). Linabeba mamlaka ya Mungu mwenyewe, na linajitafsiri lenyewe, wala halihitaji kuongezewa chochote, wala haliwezi kugeuzwa au kupinduliwa na hekima ya kibinadamu.

Neno la Mungu lililoandikwa ni rula katika maisha yetu kama wanafunzi wa Yesu na lina mamlaka ya mwisho katika Kanisa.

Linasimika, kuamsha na kuongoza utume wetu katika ulimwengu. Ushirika ambao tunaofurahia pamoja na Bwana wetu aliyefufuka na kupaa unakuzwa tunapoliamini na kulitii Neno la Mungu, na kutiana moyo sisi kwa sisi kuliruhusu kuunda kila sehemu ya maisha yetu.

Ushirika huu unaharibika tunapoliacha Neno la Mungu au tunapojaribu kulitafsiri upya kwa njia yoyote ile inayogeuza kabisa kile kilicho wazi kilichoandikwa katika muktadha ulio kanuni na hivyo kukana ukweli wake, uwazi wake, utoshelevu wake, na mamlaka yake (Tamko la Yerusalemu, Aya ya 2).

**Mgogoro Uliopo Sasa katika Ushirika wa Waanglikana Ulimwenguni (Anglican Communion)**

Licha ya jitihada zisizokoma za Maaskofu Wakuu walio wengi katika Kanisa Anglikana kwa miaka 25 ya kutoa maonyo, misingi ya Ushirika wa Waanglikana Ulimwenguni imebomolewa na tabia ya ukengeufu na kukataa mamlaka ya Neno la Mungu. Maonyo haya yamepuuzwa kwa makusudi kabisa, na kwa sasa, bila toba, mpasuko huu hauwezi kurekebishwa.

Mfano mzuri wa hivi karibuni wa tabia ya ukengeufu ni kura ya walio wengi katika Sinodi ya Kanisa Anglikana nchini Uingereza (Church of England) mwezi Februari 2023 kukubali mapendekezo yaliyotolewa na Maaskofu kwamba watu wa jinsia moja wapokee baraka za Mungu. Ni jambo linalomhuzunisha Roho Mtakatifu na sisi pia linatuhuzunisha kuona kwamba uongozi wa Kanisa Anglikana nchini Uingereza umedhamiria kubariki dhambi.

Kwa vile BWANA habariki ndoa za jinsia moja, ni jambo la udanganyifu kichungaji, na la kufuru, kutengeneza na kutumia ibada zisizofaa kubariki watu kwa jina la Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

Kukataa kufuata mafundisho ya Biblia kwamba mahali pekee pa watu kujamiana ni ndani ya ndoa inayodumu kati ya mwanamume na mwanamke (Mwanzo 2:24; Mathayo 19:4-6) ni kuvuruga mpango wa uumbaji na kuhatarisha wokovu (1 Wakorintho 6:9).

Matamshi yaliyotolewa hadharani na Askofu Mkuu wa Canterbury na viongozi wengine katika Kanisa Anglikana nchini Uingereza, wakiunga mkono suala la kubariki ndoa za jinsia moja ni usaliti kwa viapo vyao walivyotoa wakati wa kuwekwa mikono [kuwa Makasisi] na kuwekwa wakfu [kuwa Maaskofu], kwamba watalinda na kutetea ukweli unaofundishwa katika Biblia.

Matamshi hayo ya hadharani pia yanakanusha azimio namba 1.10, la Mkutano wa Lambeth wa 1998 – azimio ambalo liliweka bayana kwamba 'ushoga ni kinyume na Neno la Mungu', na kukataza kuhalalisha au kubariki ndoa za jinsia moja'.

Matamshi hayo yametolewa licha ya ukweli kwamba Askofu Mkuu wa Canterbury mwenyewe 'alithibitisha uhalali wa azimio namba 1.10 lililopitishwa na Mkutano wa Lambeth mwaka 1998 na kwamba azimio lote bado liko hai.'

Mkutano wa Lambeth wa 2022 ulidhihirisha uwepo wa mgawanyiko mkubwa katika Ushirika wa Waanglikana Ulimwenguni kwa sababu Maaskofu wengi waliamua kutohudhuria na wale [baadhi ya] waliohudhuria walikataa kushiriki Meza ya Bwana.

**Kushindwa kwa Askofu Mkuu wa Canterbury na Vyombo Vingine vya Ushirika wa Waanglikana**

Hatuna imani kwamba Askofu Mkuu wa Canterbury mwenyewe pamoja na vyombo vya Ushirika wa Waanglikana Ulimwenguni (Instruments of Communion) vinavyoongozwa na yeye (yaani Mkutano wa Lambeth, Baraza la Mashauriano la Ushirika wa Waanglikana Ulimwenguni na Mkutano wa Maaskofu Wakuu) vina uwezo wa kuonyesha njia ya kimungu kwenda mbele, ambayo itakubalika kwa wale wanaosimamia ukweli, usafi, utoshelevu na mamlaka ya Neno la Mungu. Vyombo vya maamuzi ya Ushirika wa Waanglikana vimeshindwa kulinda Ushirika ambao una misingi katika Neno la Mungu na imani ya pamoja katika Kristo.

Vyombo hivyo vyote vinne vinapendekeza kwamba njia kwenda mbele katika Ushirika wa Waanglikana Ulimwenguni ni kutembea pamoja katika 'kukubaliana kutokubaliana'. Lakini, tunakataa madai kwamba misimamo miwili inayopingana inaweza kuwa na uhahali katika masuala ya wokovu. Hatuwezi 'kutembea pamoja' kwa kukubaliana kutokukubaliana pamoja na wale ambao wameamua kwa makusudi kuachana na "Imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu" (Yuda 1:3). Watu wa Mungu 'wanatembea katika njia zake', 'wanatembea katika nuru', na yote haya yanatulazimu tusitembee katika ushirika wa Kikristo na wale walio gizani (Kumbukumbu la Torati 8:6; 2 Yohana 4; 1 Yohana 1:7).

Maaskofu Wakuu kadhaa wa Canterbury kwa mfuatano wameshindwa kulinda imani kwa kualika Lambeth Maaskofu ambao wamekumbatia au wanakuza vitendo vilivyo kinyume cha Maandiko. Hali ya kushindwa kuwa na marudi (nidhamu) ya Kanisa imechochewa sana na Askofu Mkuu wa Canterbury wa sasa, ambaye yeye mwenyewe amekubaliana na uaandaji wa ibada za kubariki vitendo vilivyo kinyume na Maandiko. Hii inafanya uongozi wake kwa Ushirika wa Waanglikana Ulimwenguni kukosa uhalali.

**Wito wa Toba**

Toba inaunda na kuelekeza maisha ya Kikristo na maisha ya Kanisa. Kila siku katika Kongamano, kwa kuitikia Neno la Mungu katika Wakolosai, tulipata muda wa kutubu.

Kwa kutambua dhambi zetu wenyewe, na kwa unyenyekevu kama wenye dhambi waliosamehewa, tunaombea wale waliokana Ukristo ulio na misingi ya Imani halisi kwa maneno au matendo, watubu na kumrudia BWANA (Tamko la Yerusalemu, Aya ya 13).

Kwa kuwa walio katika nafasi ya kufundisha [wengine] watahukumiwa zaidi (Yakobo 3:1) tunatoa rai kwa majimbo, madayosisi na viongozi wao ambao wameacha mafundisho sahihi ya Biblia kutubu kwa kushindwa kwao kusimamia mafundisho ya Biblia. Hii inahusu mambo kama vile ujinsia wa binadamu na ndoa, upekee na uungu wa Kristo, ufufuo wake kimwili, ahadi ya kurudi kwake mara ya pili, na wito wa kiimani na toba na hukumu ya mwisho.

Tunatamani kuona toba hii, lakini hadi hapo wahusika watakapotubu, ushirika wetu pamoja nao umevunjika.

Tunahesabu kwamba wale wanaokataa kutubu wametelekeza haki yao ya uongozi katika Ushirika wa Waanglikana Ulimwenguni, nasi tunajitolea kufanya kazi na Maaskofu Wakuu na viongozi wengine wanaoshika mafundisho sahihi kuunda upya Ushirika wa Waanglikana katika misingi yake ya ki-Biblia.

**Kuunga Mkono Waanglikana Waaminifu**

Tangu Gafcon ilipoundwa, imelazimu Maaskofu Wakuu wake kutambua maeneo mapya kiutawala ambako kuna Waanglikana waaminifu kama vile Kanisa Anglikana Amerika Kaskazini (ACNA), Kanisa Anglikana Brazil, Mtandao wa Kanisa Anglikana Ulaya, Kanisa la Waanglikana Wanaokiri Imani Sahihi (Confessing Anglicans) walioko Aotearoa New Zealand, na Dayosisi ya Southern Cross [Australia]. Tunahimiza Maaskofu Wakuu kuendelea kutoa usalama wa aina hiyo kwa Waanglikana waaminifu.

Kutokana na hali ya mgogoro wa sasa, tunarudia kuunga mkono wale ambao hawawezi kubaki katika Kanisa Anglikana nchini Uingereza kwa sababu ya kushindwa kwa uongozi wa Kanisa hilo. Tunafurahia kukua kwa ANiE (Anglican Network in Europe/ Mtandao wa Kianglikana Ulaya) na mitandao mingine ambayo inafungamana na Gafcon.

Aidha tunaendelea kuwaombea na kusimama pamoja na Waanglikana waaminifu ambao wameamua kubaki katika Kanisa Anglikana nchini Uingereza. Tunaunga mkono juhudi zao za kusimamia Imani sahihi ya ki-Biblia na kupinga kwao uvunjaji wa Azimio 1.10 [la Lambeth].

**Uchungaji Unaofaa**

Hali tukitambua dhambi zetu na udhaifu wetu, tunakubali kutoa uchungaji unaofaa kwa watu wote katika makanisa yetu. Hii ni muhimu sana katika mazingira ya sasa ya mchanganyo kuhusu ujinsia na jinsia, ambao umevurugwa sana na ukuzaji wake wa kimfumo duniani kote.

Uchungaji unaofaa unathibitisha uaminifu katika ndoa na kutojamiana katika useja.

Sio jambo jema kichungaji kuwapotosha watu, kwa kujifanya kwamba Mungu anabariki uhusiano wa watu wawili wa jinsia moja wanaofanya tendo la ngono au kujamiana. Huu sio upendo kwa sababu unafanya watu hao wakosee na kuwawekea kikwazo katika njia yao ya kurithi ufalme wa Mungu (1 Wakorintho 6:9-11).

Tunakiri kwamba kila mtu anapendwa na Mungu, na tumedhamiria kuwapenda watu kama Mungu anavyowapenda. Kama Azimio 1.10 [la Lambeth] linavyosema, tunapinga unyanyasaji na udhalilishaji wa mtu yeyote aliyeumbwa kwa mfano wa Mungu, na hii ni pamoja na kuwapenda wale wasiofuata njia za Mungu kwa sababu kila mtu ameumbwa kwa mfano wa Mungu.

Tunamshukuru Mungu kwa ajili ya wote wanaojitahidi kuishi maisha yenye uaminifu kwa Neno la Mungu katikati ya majaribu ya ngono.

Tunaahidi upya kusaidiana na kutunzana katika upendo na kwa namna inayotambua haja ya kichungaji kama watu walio sehemu ya mwili wa Kristo, kujengana katika Neno na katika Roho, na kutiana moyo sisi kwa sisi kupokea nguvu ya Mungu yenye uwezo wa kubadilisha maisha kadri tunavyotembea kwa imani katika toba na utii unaofikisha mtu katika utimilifu wa maisha.

**Kuunda Upya Ushirika wa Waanglikana Ulimwenguni**

Tulifurahishwa kwamba viongozi wa Ushirika wa Waanglikana Kusini mwa Dunia (Global South Fellowship of Anglicans – GSFA) waliungana nasi Kigali, na sisi tulikuwa wenyeji wa mkutano wa pamoja wa Maaskofu Wakuu wa Gafcon na GSFA. Kwa pamoja hawa Maaskofu Wakuu wanawakilisha idadi kubwa zaidi (takriban 85%) ya Waanglikana duniani kote.

Viongozi wa makundi yote mawili walithibitisha na kufurahia wajibu wao wa kutegemeana katika Ushirika wa Waanglikana Ulimwenguni.

Gafcon ni ushirika ambao unajikita zaidi katika Uinjilisti na Utume, kufungua makanisa mapya na kutoa msaada na kimbilio kwa Waanglikana waaminifu wanaopata msukosuko, au wanaofukuzwa kutoka katika madayosisi na majimbo yenye ukengeufu wa kiimani. Kwa upande mwingine, GSFA inajikita katika uundaji wa mifumo yenye mamlaka itakayosimamia mafundisho sahihi ndani ya Ushirika wa Waanglikana Ulimwenguni.

Tunafurahia tendo la makundi yote mawili kuahidi kusimamia na kujitolea kwa pamoja kuhusu mambo matatu: ukuu wa Yesu Kristo; mamlaka na usafi wa Neno la Mungu; na kanisa kuweka kipau mbele suala la utume kwa ulimwengu. Tunatambua makubaliano yao kwamba msingi wa 'ushirika' baina ya makanisa na Wakristo ni mafundisho sahihi (Tamko la Yerusalemu Na. 13; Agano la GSFA Na. 2.2.6). Utambulisho wa Kianglikana (Anglican Identity) unatokana na ukweli huu, na wala sio kwa kutambuliwa na Dayosisi ya Canterbury.

Maaskofu Wakuu wa Gafcon na GSFA wana msimamo wa pamoja kwamba kutokana na kuachwa kwa imani sahihi ya ki-Biblia kama ilivyoelezwa hapo juu, hawawezi kuendelea kutambua Askofu Mkuu wa Canterbury kama alama ya umoja katika Ushirika wa Waanglikana Ulimwenguni, wala hastahili kuwa na nafasi ya pekee miongoni mwa Maaskofu Wakuu. Kanisa la Uingereza limeamua kuharibu uhusiano wake na majimbo yenye Imani sahihi katika Ushirika wa Waanglikana.

Tunapokea kwa ukunjufu Tamko la GSFA walilotoa siku ya Jumatano ya Majivu tarehe 20 Februari 2020, wakitoa rai kwamba Ushirika wa Waanglikana Ulimwenguni uundwe upya. Tunasifu mwaliko uliotolewa na Maaskofu Wakuu wa GSFA wa kushirikiana na Gafcon na makundi mengine yenye imani sahihi kufanyia kazi suala la muundo na namna bora ya maisha yetu pamoja na jinsi gani tunavyoweza kudumisha kipau mbele cha kutangaza Injili na kuwafanya watu kuwa wanafunzi wa Yesu katika mataifa yote.

Suala la kuunda upya Ushirika wa Waanglikana Ulimwenguni ni jambo la haraka sana. Linahitaji msingi imara na wa kutosha kushughulikia masuala ya kisheria na ya kikatiba katika majimbo mbalimbali. Lengo kuu ni kwamba Waanglikana wenye imani sahihi wawe na utambulisho unaoeleweka, mahali patakapokuwa kama 'nyumba ya imani' ya kimataifa, mahali ambapo wataona fahari juu ya mfumo wa uongozi unaowapa uimara na mwelekeo kama Waanglikana kimataifa. Kwa hiyo tunaahidi kuomba kwamba Mungu aweze kuongoza mchakato huu wa kuunda upya [Ushirika wa Waanglikana], na kwamba Gafcon na GSFA wataenenda katika Roho Mtakatifu juu ya suala hili.

**Mustakabali Wetu Pamoja**

Tulipotafakari mustakabali wa Ushirika wetu, tulipokea vipau mbele saba vifuatavyo vilivyotolewa na Katibu Mkuu [wa Gafcon] na kuidhinishwa na Maaskofu Wakuu wa Ushirika wa Gafcon.

Tutashiriki katika **muongo wa kufanya wanafunzi wa Yesu, Uinjilisti na Utume (2023-2033).**

Tutajikita katika kuinua **viongozi wa kizazi kijacho** katika Gafcon kupitia elimu ya theolojia iliyo na msingi katika Biblia, na ambayo itawajenga ili wafanane na Kristo na wawe na moyo wa utumishi.

Tutaweka kipau mbele kwenye **huduma ya vijana na watoto** ambayo itawafundisha Neno la BWANA, na kuwafanya wawe wanafunzi wa Yesu waliokomaa kiroho ndani ya Kristo, huduma ambayo pia itawajenga katika utumishi wa kikristo unaodumu.

Tutakubali na kukuza huduma muhimu na zilizo tofauti ikiwa ni pamoja na nafasi mbali mbali za uongozi wa **wanawake katika Gafcon** kwenye ngazi ya familia, Kanisa na jamii, iwe ni mtu mmoja mmoja au katika vikundi.

Tutaonyesha kwa vitendo huruma ya Kristo kupitia **huduma za faraja katika Gafcon**.

Tutaweka rasilimali na kuunga mkono **mafunzo kwa Maaskofu** ambayo yatazaa viongozi waaminifu, wenye ujasiri na wenye moyo wa utumishi.

Tutajenga ushirika ulioshikamana na utakaonufaisha pande zote baina ya Jimbo na Jimbo kupitia katika ziara za Maaskofu Wakuu.

Kutokana na mkutano wetu huu, tunawatia moyo Maaskofu Wakuu nao watoe kipau mbele kwa suala la kuwafanya vijana na wanaume watu wazima kuwa wanafunzi wa Yesu.

Ili kutekeleza vipau mbele hivi na kukuza kazi ya Ushirika wa Gafcon, tumekubaliana na wazo la kuanzishwa kwa mfuko wa fedha utakaotokana na michango. Aidha tunatia moyo Majimbo ya Gafcon kujitahidi kujitegemea kifedha, sio tu katika kuendelezea kazi ya utume, lakini pia kuepuka kurubuniwa na fedha.

Mwisho kwa umuhimu wa pekee, tunajitoa upya kusimamia utume wa Kiinjili wa kumtangaza Kristo aliyesulubiwa, aliyefufuka na kupaa mbinguni, huku tukiwataka watu wote kumkubali kama BWANA kwa njia ya toba na imani, na kuishi maisha yenye furaha na utii wenye uaminifu kwa Neno lake katika maeneo yote ya maisha yetu. Tutatafuta njia mpya za kutiana moyo, kuombeana, na kuwajibishana katika masuala haya.

Tunajikabidhi katika mikono ya Baba yetu wa mbinguni na mwenye upendo huku tukiwa na imani kwamba Yeye atatimiza ahadi zake zote, na hata katika nyakati za kupogoa (yaani kupunguza majani katika mti), Kristo atalijenga Kanisa lake.

**“Twende kwa Nani”**

Tunaenda kwa Kristo ambaye yeye peke yake anayo maneno ya Uzima wa milele (Yohana 6:68)
na kisha tukiwa na Kristo tufikie ulimwengu mzima. Amin.